



# TAARIFA YA MKUTANO WA MWAKA KWA Wawekezaji wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

TAREHE: 15, 16 NA 17 NOVEMBA, 2024

Taarifa na ratiba inatolewa kwa ajili ya Mikutano ya Mwaka kwa Mifuko ya uwekezaji wa pamoja itakuwa kama ifuatavyo:

JINA LA MFUKO	MUDA	TAREHE	SEHEMU/UKUMBI
Umoja	Saa 2:30 Asubuhi	15 Novemba, 2024	Mikutano yote itafanyika katika: Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam
Wekeza Maisha	Saa 8:00 Mchana	15 Novemba, 2024	
Ukwasi	Saa 2:30 Asubuhi	16 Novemba, 2024	
Kujikimu	Saa 8:00 Mchana	16 Novemba, 2024	
Hatifungani	Saa 2:30 Asubuhi	17 Novemba, 2024	
Watoto	Saa 8:00 Mchana	17 Novemba, 2024	

Ajenda za mikutano hiyo ni pamoja na:

1. Kufungua Mkutano;
2. Kupitia na kupitisha dondoo za mkutano uliopita;
3. Kupata taarifa za yatokeo kutoka kwenye mkutano uliopita;
4. Kupitia na kupitisha taarifa za hesabu za Mfuko kwa mwaka wa 2023/2024;
5. Taarifa ya Uwekezaji kutoka kwa Meneja wa Mfuko kwa Mwaka wa 2023/2024;
6. Mengineyo.

Wawekezaji wanaalikwa kuhudhuria Mkutano Mkuu wa Mwaka kwa Mifuko iliyotajwa hapo juu. Wawekezaji wanaombwa kufika katika Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam [siku na muda kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapo juu], akiwa na kitambulisho (cha taifa/cha kupiga kura/leseni ya udereva/hati ya kusafiria). Mkutano huu utakuwa kwa njia ya mtandao pia, maelekezo ya kujisajili kwa njia ya mtandao yatatumwa kwa njia ya ujumbe wa simu kwa wawekezaji wote.

UTT AMIS - Meneja wa Mifuko  
Mkurugenzi Mtendaji

#### Muhimu:

- Kama kuna maoni/mapendekezo/maswali yawasilishwe kwa Meneja wa Mfuko (UTT AMIS) kabla ya tarehe 4 Novemba, 2024 kwa kutumia S.L.P 14825, DSM au uwekezaji@uttamis.co.tz
- Washiriki katika mikutano hii watawajibika kujigharamia wenyewe.